# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA VIJIJINI

## SHULE YA SEKONDARI KILANGALANGA
## MLANDIZI - PWANI

FOMU YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO
MWAKA 2023/24

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBAHA**

**Mawasiliano**;
**Mkuu wa Shule: 0787 442 428**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0620 515 045**

**SHULE YA SEKONDARI KILANGALANGA**
**S.L.P 177,**
**MLANDIZI**

KUMB.NO KSS/F. V 2023/2024/01

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi…………………………...
…………………………………………………………….
S.L.P.……………….……………………………………

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO MWAKA WA MASOMO 2023/2024 KATIKA SHULE YA SEKONDARI KILANGALANGA ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA, MKOA WA PWANI.**

1.0 Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari kidato cha tano katika shule hii. Unapaswa kufika shuleni tarehe………………………. Kabla ya saa 11 jioni muda wa kazi bila kukosa. Shule ipo Mlandizi umbali wa kilomita 1½ kutoka unaposhukia stand ya mji mdogo wa Mlandizi. Usafiri wa kufikia Shuleni unapatikana muda wote na unaweza kupanda pikipiki kwa shilingi 500/= - 1000/= au Tax kwa Tsh 2,000/= hadi 2,500/=

2.0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**
A. **MICHANGO YA SHULE**
Fedha zinazohusu michango ya shule zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na, **21201200105 katika Benki ya NMB. (Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye bank payment slip)**

B. Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi ni -:

**Michango mbalimbali**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Angalizo: Jumla ya michango kwa wanafunzi wa bweni ni shilingi 80,000/=**
**(Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Na.21201200105 katika benki ya NMB.**

Shule haipokei fedha taslimu fedha zote zilipwe kupitia benki ya NMB tawi lolote kwa kutumia namba za akaunti husika na stakabadhi za malipo (Bank Payment Slip) zenye jina kamili la mwanafunzi ziletwe shuleni siku ya kuripoti. Tafadhali rejea mfano wa ulipaji katika “bank pay slip” kama ilivyoambatanishwa.

## 2.2 SARE YA SHULE

2.2.1 Suruali mbili (2) rangi ya kijivu St. Marry pana zisiwe "modo", iwe na marinda pamoja na turn up mguuni. ( **Atashonewa baada ya kufika shuleni ili kuwa na mfano wa sare kwa wanafunzi wote**)
2.2.2 Mashati meupe mikono mifupi mawili (2) (**aje nayo mwanafunzi siku ya kuripoti**)
2.2.3 Soksi nyeusi jozi mbili (2) rangi nyeusi
2.2.4 Viatu vya kufunika vya Kamba vyeusi jozi mbili (2)
2.2.5 Sweta yenye shingo V rangi ya kijani kwa wanaohitaji.
2.2.6 Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa Ngozi.
2.2.7 Tai mbili kitambaa cha kijivu cha suruali ya shule.

## 3.0 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI:-

3.1 Bunda (ream) za karatasi mbili (2) kwa kila mwaka.
3.2 Raba za michezo pea moja (1)
3.3 Shuka nne (4) rangi ya blue (zitakaguliwa siku ya kuripoti)
3.4 Mto na foronya rangi ya blue
3.5 Ndoo 1 ndogo kwa ajili ya kufulia nguo,na dumu dogo (lita 5) kwa ajili ya kutunzia maji
3.6 Kijiko 1, bakuli 1, sahani 1, na kikombe kimoja kwa ajili ya chakula.
3.7 Tochi ya betri kwa tahadhari ya umeme ukikatika isiwe ya kuchaji
3.8 Madaftari makubwa (Counter books) angalau 10 au Zaidi kwa ajili ya masomo
3.9 Scientific calculator kwa wanafunzi wa science
3.10 Kitambulisho cha bima ya afya kama unacho
3.11 Mwamvuli kwa tahadhari ya mvua wakati wa masika.
3.12 koti la maabara jeupe kwa wanafunzi wa **PCB** na **PCM** (aje nalo)
3.13 Stop watch kwa ajili ya kutumia kwenye practical.
3.14 Godoro jipya futi 2.5
3.15 Chandarua mpya ya rangi ya Blue (Pembe nne)
3.16 **Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuja na nguo za nyumbani Shuleni** hivyo anatakiwa kuwa na nguo zifuatazo kwa ajili ya kushindia awapo hapa shuleni mda wote na zinatakiwa kuwa za kufanana

- Track suit ya blue yenye michirizi meupe.
- T-shirt ya blue.
- Nembo ya shule (**inapatikana shuleni)**
- Bukta ya blue anakuja nayo.
- Pia unatakiwa kuja na T-shirt ya kushindia ya round rangi ya damu ya mzee isiwe na maandishi yeyote.
- Suruali nyeusi anakuja nayo

3.17 Flat file
3.18 Dissecting kit kwa wanafunzi wa **PCB** aje nayo.

## 4.0 VIFAA VYA USAFI

**Kwa wanaliopangiwa tahasusi ya PCM wanapaswa kuja na vifaa vifuatavyo:-**

4.1 Fagio la ndani lenye mpini mrefu (Soft broom) 1
4.2 Reki 1
4.3 Chelewa ndefu ya nje (Fagio la wima) 1
4.4 Squeezer 1 (mpira wa kukaushia maji)
4.5 Panga 1

**Kwa wanaliopangiwa tahasusi ya PCB wanapaswa kuja na vifaa vifuatavyo:-**

4.5 Fagio refu la buibui 1
4.6 Brashi ya kusugulia choo yenye mpini mfupi 1
4.9 Jembe pamoja na mpini wake 1
5.0 Fagio la ndani lenye mpini mrefu (Soft broom) 1
5.1 Chelewa ndefu ya nje (Fagio la wima) 1

## 5.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu history ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha tano (5) za wazazi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu,Rejea kiambatanisho D kipengele cha 12.
e) Copy ya cheti cha kuzaliwa
f) Copy ya "Result slip"

NB: SHULE ITAKUWA NA SIKU YA WAZAZI (**PARENTS' DAY**) KILA JUMAMOSI YA KWANZA YA MWEZI WA KUMI KILA MWAKA. TUOMBE WAZAZI KUTENGA MUDA WENU KILA IFIKAPO SIKU TAJWA KUFIKA SHULENI KUJADILI MAMBO MTAMBUKA KUHUSIANA NA SHULE NA WATOTO WETU HUSUSANI MAENDELEO YA TAALUMA

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA**

**"WILL, POWER AND PERSEVERANCE"**
**PENYE NIA PANA NJIA**

**……………………………………………**
**MKUU WA SHULE**

**KIAMBATANISHO A**

## HATI YA MAKUBALIANO

### YAH: HATI YA KUKUBALI MASHARTI YA KUSOMA SHULE YA KILANGALANGA SEKONDARI.

Mimi …………………………………………nakubali nafasi ya kidato cha………………………. niliyopewa katika shule yako.

Ninayakubali masharti na kuwa nitatii sheria za shule hizo zilizopo na kuwatii walimu wote wa shule na wafanyakazi kama walezi wangu.

Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mwaminifu. Naahidi pia kuwa nitajielimisha kwa nguvu zangu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu.

Natambua kuwa nikikiuka ahadi hizo nitapoteza nafasi yangu hapa shule.

JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………...SAHIHI ……………… TAREHE……

JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………. SAHIHI……………… TAREHE…….

**KIAMBATANISHO B**

### FOMU YA KIAPO CHA MWANAFUNZI KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO PAMOJA NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi……………………………………………………………. Kidato cha …………………….
Nimekubali nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Kilangalanga. Ninaahidi kuwa mtiifu na kufuata kikamilifu **SHERIA, KANUNI**, TARATIBU **na MIONGOZO** halali zilizopo.Pia ninaahidi kufanya bidii na kushirikiana na uongozi wa shule na wanafunzi wenzangu katika kuendeleza taaluma na shughuli nyingine nitakazopangiwa. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo pamoja na makosa ya jina.

JINA LA MWANAFUNZI……………………. SAHIHI……………TAREHE……………………

## KIAMBATANISHO "C"

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi……………………………………………………………………………………………………..

1. Nimesoma na kuelewa sheria,taratibu na miongozo ya shule kwenye fomu hii na nimekubali kujiunga na shule hii ya sekondari…………………………………Kuanzia tarehe……………...
2. Naahidi kuwa:-
   a) Nitazingatia sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.
   b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na Sheria za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
   c) Nitatunza mali ya Umma ambayo ni pamoja na Majengo,Samani,Vitabu na Vifaa vya maabara.
   d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yeyote stahiki endapo nitakiuka maelekezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

   Saini ya Mwanafunzi……………………………….Tarehe………………………………

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mzazi/mlezi wa ……………………………………………………kidato cha ………………………….

Naahidi kuwa:-

1) Nitashiriki kikamilifu na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla katika kumuelimisha na kumlea motto wangu. Hiini kuhakikisha kuwa atazitii Sheria zote za shule na kuyazingatia mambo yote muhimu yaliyotajwa.
2) Nitafanya ufuatiliaji wa maendeleo ya Mwanafunzi kipindi chote atakachokuwepo shuleni.
3) Naruhusu Mwanangu achukuliwe hatua yeyote stahiki endapo atavunja sheria na kanuni zilizoorodheshwa.

   Saini ya Mzazi/Mlezi……………………………………Tarehe………………………………..

**KIAMBATANISHO D.**

## FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUMZI

1. Jina kamili la Mwanafunzi.......................................................................
2. Dini ........................................Dhehebu....................................................
3. Tarehe ya kuzaliwa..................................Mahali.........................................
4. Jina la Baba.......................................................Hai/Amefariki...............
5. Jina la Mama.......................................................Hai/Amefariki...............
6. Je una Wazazi wako wote? Ndio/Hapana....................................................
7. Kama hapana je unaishi na nani?...............................................................
   Jina lake unaeishi nae.......................................................................
   Uhusiano wake na wewe?...........................................................................
8. Kidato unachokuja kuingia hapa shuleni....................................................
9. Michezo unayopendelea kushiriki ukiwa shuleni.
   i. ......................................
   ii. ......................................
   iii. ......................................
10. Je umewahi kuwa kiongozi/kiranja? Ndio/hapana.............................
    Kama jibu ni ndio eleza ulikuwa kiongozi/kiranja wa nini?............................
    .....................................................................................................................................
    ..........................................................................
11. Taja mambo mengine unayopendelea kufanya nje ya masomo............
    i. ................................................
    ii. ................................................
    iii. ................................................
12. **ORODHESHA MAJINA YA NDUGU WA KARIBU (WA KIKE/KIUME)**

    **Angalizo**: Ndugu wawili wa juu awe ni Baba au Mama au walezi anaokaa nao pia endapo mzazi/mlezi utabadilisha mawasiliano(Namba ya simu) utapaswa pia kutoa taarifa Shuleni ili kubadilisha taarifa za Mwanzo au Mwanafunzi ulikuwa unakaa nae akaondoka kwako na kwenda kukaa kwa ndugu mwingine pia utapaswa kutoa taarifa ofisi ya usajili iliyompokea mwanafunzi wakati anajiunga na shule.

| Na. | Jina la Ndugu | Uhusiano | Kazi yake | Na. ya simu |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |

**Nadhibitisha kwamba taarifa nilizotoa hapo juu ni sahihi**

**Saini ya Mwanafunzi...............................................Tarehe..............................**

**Attachment No: E**

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS**
**KIBAHA DISTRICTS COUNCIL**

***FROM:***
**HEAD OF SCHOOL**
KILANGALANAGA SECONDARY
P.O.BOX 177, Mlandizi

**The Medical Officer………………………………………………………**
**(GOVERNMENT M.O)**

Name of Students…………………………………………………………………………Date………………………
Term ……………………… Year……………………… i shall be very grateful if you will kindly examine the above-named student and give use a report regarding his/her fitness to undertake studies well in our school. The following examination indicated by X in bracket is especially:

## A. PRELIMINARY INFORMATION MEDICAL HISTORY

| NO | DISEASE | YES | NO | | DISEASE | YES | NO | | DISEASE | **YES** | **NO** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | | 7 | Numerous Breakdown | | | 13 | V.D | | | |
| 2 | Asthma | | | 8 | Ear/Noise/Throat Trouble | | | 14 | Disabled | | | |
| 3 | Pneumonia | | | 9 | Skin disorder/Disease | | | | | | | |
| 4 | Heart | | | 10 | Anemia | | | | | | | |
| 5 | Recurrent | | | 11 | Operation | | | | | | | |
| 6 | Jaundice | | | 12 | Eye Disorder | | | | | | | |

## B. VITAL STATISTICS

Age…………………height………………weight…………………blood group………
BLOOD PRESSURE……………………………PURSE RATE…………………………………..
SYSTOLIC………………………………………… DIASTOLIC……………………………

## C. MEDICAL EXAMINATION

| | **REMARKS/TREATMENT** |
|---|---|
| **EAR** | **RT ………………  LT……………** |
| **VISION** | **RT.EYE……………………LT.EYE……………** |
| **THROAT** | |
| **CHEST EXAMINATION** | |
| **ABDOMINAL EXAM** | **LIVER  SPLEEN** |
| | **OTHER COMMENTS** |
| **M.S SYSTEM** | **UPPER LIMBS** |
| | **LOWER LIMBS** |
| | **SKIN** |
| **ANY OTHER FIND** | |

## D. LABORATORY EXAMINATIONS/INVESTIGATION

1) **STOOL: Ova……………………………………………………………leucocytes**
2) **URINALYSIS: PROTEIN………………………………………………………**
   **GLUCOSE………………………………………………………….**
   **SEDMENT: - OVA……………………………………leucocytes**
3) **HB……………………………………………………………………………….**
4) **B/S……………………………………………………………………………..**
5) **VDRL……………………………………………………………………………**
6) **WBC TOTAL…………………………………………………………….**
   **DIFFERENTIAL……………………………………………….**
7) **X-RAY CHEST……………………………………………………………….**
8) **ANY OTHER INVESTS………………………………………………………..**

## E. MEDICAL CERTIFICATE:

**We request the medical office to complete the following**
I have examined the above-named student and considered that he/she is physically fit for most activities takes at the school that he/she gets further treatment that my finding as indicated above.

Date……………………..Station…………………DR. S NAME ………………. SIGNATURE

**Thank you in advance**

……………………………
**The Headmaster**
**KILANGALANGA SECONDARY SCHOOL**

**KIAMBATANISHO F**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA**

**MAAGIZO MUHIMU YA VITABU VYA KIADA NA ZIADA**

Ili mwanafunzi aweze kupata elimu bora yenye kumwezesha kukabiliana na mazingira halisi, anapaswa kuwa na vitabu. Hapa ni baadhi ya vitabu ambavyo anapaswa kuja navyo ili aweze kumudu sawa sawa mchepuo wake.

1. **GENERAL STUDIES**
   - I. Mgawanyo B.M -
   - II. Nyangwine A -
   - III. Ahmadiyya -

   General studies for Advance Level, Notes for general studies form five and six Communication skilled, theory and practical

2. **PHYSICS**
   - I. Nelkon and Parker - Principal Physics
   - II. Roger, M - Physics
   - III. Kiiza R - Solved major problem in Physics
3. **BIOLOGY**
   - I. Michael R - Advance Biology for secondary school
   - II. Taylor O.J. Stoud G.W - Biology science
   - III. Msaky, L - Cell structure and organization
4. **CHEMISTRY**
   - I. Roms, D - A level chemistry
   - II. Mzumbe project - inorganic chemistry
   - III. Brown - physics chemistry
5. **ADVANCE MATHEMATICS**
   - I. Shayo - advanced mathematics
   - II. Tranra J. - advanced mathematics
   - III. Chandi, S - mathematics studies and probability

**"WILL POWER PERSEVERANCE**
**"PENYE NIA PANA NJIA"**

………………………………………………
**MKUU WA SHULE**

# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI KILANGALANGA

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

**UTANGULIZI**

Shule ya sekondari Kilangalanga ni taasisi ya Elimu ambapo wanakaa na kuishi walimu na familia zao, wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi.

Pia katika eneo jirani na shule wapo wanajamii wa mtaa wa Kilangalanga. Licha ya taratibu za kawaida za kuishi katika jamii pamoja na kanuni na sheria za nchi, kila mwanafunzi atatakiwa kufuata taratibu/sheria za shule/wizara ya Elimu kama ifuatavyo:

**A: HESHIMA**

Katika kutekeleza suala zima la heshima shuleni yafuatayo yanatakiwa yazingatiwe:

i) Kila mwanafunzi anatakiwa kusimamia na kuheshimu Mwalimu au mtu yoyote aliyemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

ii) Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya na isiyo na heshima wakati wowote kati yake na mwanafunzi mwenzake,kwa walimu wake au kwa mtu mwingine yeyote.

iii) Kila mwanafunzi anatakiwa ashirikiane vizuri na kuwatii walimu wake na wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.

iv) Kila mwanafunzi anatakiwa ashirikiane vizuri na wanafunzi wenzake katika kazi halali za shule. Pia kila mwanafunzi anatakiwa kuthamini kazi za aina zote zinazotolewa shuleni.

v) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-

   a) Kutumia madawa ya kulevya
   b) Kutumia bangi, Mirungi, Vileo vya aina yoyote na sigara.
   c) Kufuga kucha,Ndevu,Nywele zisizo safi na kusuka Rasta.
   d) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima kama vile Nguo zinazobana mwili,Singlet zilizokatwa na zilizo chorwa chorwa. Pia kukunja mikono ya shati, fulana na suruali.
   e) Kumkimbia Mwalimu au mfanyakazi wa shule.
   f) Kubishana na Mwalimu na kuto mtii atoapo maagizo halali.
   g) Kutotii kengere ya shule.
   h) Kudharau na kukejeri Mwalimu, wafanyakazi wasio walimu na viranja (viongozi wa wanafunzi)

i) Kugombana na mwanafunzi mwenzako au mtu yeyote.
j) Kuhifadhi silaha kama Nondo, visu na vitu vingine vinavyotishia amani na usalama.

vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kuitikia mara moja na kukimbilia aliko mkuu anae waita.

vii) Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya taifa,Court of arms, wimbo wa taifa, Nyimbo za Tazama ramani,Tanzania nakupenda , wimbo wa shule na Fedha.

viii) Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu darasa, ukumbi wa mikutano,Ofisi za shule, ukumbi wa chakula, jiko, mali yake binafsi na mali ya Umma.

ix) Kila mwanafunzi anatakiwa kujipanga kwenye mstari wakati wa kupokea huduma kama chakula n.k.

x) Kila mwanafunzi anatakiwa kujipanga kwenye mstari, na kuwa mtulivu na kufuata maelekezo ya walimu na viongozi (viranja)

xi) Mwanafunzi anatakiwa kuto toa lugha yoyot ya matusi kwa mtu na kutofanya vitendo vyovyote na ishara zinazo ashiria kumdhalilisha mtu au jinsia.

xii) Kila mwanafunzi anatakiwa kumheshimu Mwalimu na wafanyakazi wote bila kujali tofauti za kisiasa, kidini na kitamaduni katika jamii pia bila kujali jinsia, rangi, na maumbile na ulemavu.

## B: MAHUDHURIO

i) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi (masomo) vyote darasani na vya nje ya darasa bila kukosa kwa kadri ya ratiba ya shule.

ii) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria na kufanya mazoezi na majaribio yote, mitihani yote ya ndani na ya kitaifa.

iii) Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki katika kufanya kazi za mikono.

iv) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule kama Baraza la shule, Ukaguzi wa usafi, Kupandisha bendera ya taifa, Mikutano ya Mabweni, mikutano ya darasa, Michezo n.k.

v) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano na makongamano ya vyama vya masomo, vyama vya huduma za kijamii na Mijadala.

vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalio ya jioni bila kukosa (evening preparation)

**N.B: MAANDALIO YA JIONI (EVENING PREPARATION):Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalio ya jioni (evening preparation) bila kukosa. Maandalio ya jioni** *yanaanza saa 1:30 usiku mpaka saa 4:00 usiku* **kila siku, kwa siku za Juma tatu, Juma nne, Juma tano, Alhamisi, Ijumaa na Juma Mosi. Juma Pili ni hiari kwa mwanafunzi.**

## C: KUWAHI

Kila mwanafunzi anatakiwa kujenga tabia ya kutunza na kuthamini muda wakati wote akiwa shuleni, na hivyo kutimiza yafuatayo.

i) Kuamka mapema Alfajiri, kufanya usafi, kufanya mazoezi ya kuchangamsha mwli na kuoga maji.
ii) Kushiriki shughuli za usafi ndani ya mda uliopangwa.
iii) Kuwahi katika shughuli za shule kama vile Mstarini, darasani,maandalio ya jioni,ukumbi wa chakula,usafi bwenini, usafi darasani na viunga nya shule.
iv) Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi kila apatapo taarifa ya kuitwa na walimu wake.
v) Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi anaposikia wito wa dharula.
vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni na kuripoti ofisi ya malezi kwa tarehe iliopangwa kufungua shule, kila baada ya likizo na sio tarehe baada ya kufungua shule.

## D: SARE YA SHULE

Wanafunzi wanapaswa kufahamu ya kwamba, sare ya shule ni fahari, ni kiunganishi chao, ni utambulisho wao, ni heshima yao katika jumuiya ya shule na jumuiya zote nje ya shule. Sare ya shule inatakiwa ivaliwe kwa heshima wakati wote wa:-

i) Masomo darasani
ii) Mwnafunzi anapotoka nje ya shule kwa shughuli zake na zile za kishule
iii) Baraza, mikutano na sherehe shuleni
iv) Mwanafunzi anapokwenda hospital
v) Mwanafunzi anapokwenda kwenye maandamano
vi) Mwanafunzi anaposafiri kuja shuleni au kwenda likizo
vii) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa mavazi ya kazi za mikono wakati wa kazi za mikono na sio sare ya shule
viii) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa mavazi ya michezo wakati wa michezo mbalimbali shuleni.

## E: UMEME

i) Ni marufuku kwa mwanafunzi yoyote kufanya uunganishaji wowote wa umeme katika maeneo ya mabwenini, darasani na jikoni.
ii) Mwanafunzi atawajibika na ulipaji wa ghalama zote zitokanazo na uunganishaji wa umeme kiholela (Illigal Connectios)
iii) Ni lazima mwanafunzi kutoa taarifa juu ya uunganisha wa umeme usio rasmi.
iv) Viongozi wa mabweni wanahusika katika ukaguzi wa mifumo ya umeme kila wakati na kutoa taarifa wanapogundua upo uunganishaji usio rasmi.

## F: MITIHANI

a) Mitihani ni kipimo cha uelewa wa mwanafunzi katika masomo yake anayosoma shuleni. Mwanafunzi anapimwa kwa maswali ya mitihani ili Mwalimu aweze kufahamu ni kwa kiasi gani ameyaelewa alioyafundisha. Mwanafunzi anatakiwa kuingia darasani na kusikiliza vipindi vyote ili aweze kufanya mitihani yake na kufaulu.
b) Unatakiwa kufanya mitihani na majaribio yote kwa kadri itakavyoainishwa katika ratiba ya shule, bila kukosa. Ni kosa kubwa sana kutokufanya majaribio na mitihani inayoandaliwa shuleni. Aidha adhabu ya kukosa kufanya mitihani ni kama ifuatavyo
    1. Onyo kali
    2. Kufukuzwa shule

Mwanafunzi hatakiwi kufanya yafuatayo:-

i) Kuogopa mitihani hivyo kutofanya mitihani kwa visingizio
ii) Kuiba mtihani au kuibia katika mtihani/jaribio
iii) Kuchagua masomo ya kufanya mitihani na kuacha mengine
iv) Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani.

## G: MAZINGIRA

Mazingira ni kila kitu kinachotuzunguka. Katika mukutadha wa hasa utunzaji wa miti, maua, nyasi na mipango endelevu ya kupanda miti na kuzuia mmomonyoko wa udongo katika shule yetu.

Katika majukumu haya hapo juu na mengine yanayohusiana na mazingira katika shule yetu, kila mwanafunzi:-

i) Anatakiwa kushiriki katika kuyatunza, kuyahifadhi na kuyaendeleza mazingira ya shule yetu.
ii) Kujielimisha kuhusu majukumu ya kuendeleza mazingira ya shule kupitia wanamazingira, vitabu/vijarida na walimu walioko shuleni.
iii) Kushiriki katika kupanda miti maua na nyasina kuvitunza vizuri kwa mbolea na maji kwa manufaa ya shule.
iv) Kila mwanafunzi anatakiwa kuyathamini mazingira ya shule kwa kutoyaharibu kwa namna yoyote ile.
v) Mwanafunzi hatakiwi kukatiza viwanjani.
vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kutoa mawazo na taarifa za kuendeleza mazingira ya shule.
vii) Mwanafunzi hatakiwi kutupa taka ovyokatika maeneo ya darasani,jikoni, bwenini na maeneo yote ya shule.
viii) Ni marufuku kukojoa au kuoga katika vichaka.

ix) Ni marufuku kutiririsha maji machafu kutoka madarasani na mabwenini.

x) Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na vitu vya plastiki isipokuwa ndoo tu.

xi) Kila mwanafunzi anatakiwa kula chakula katika bwalo tu au maeneo ya jirani na bwalo.

## H: USAFI

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia usafi wa mwili wake kwa kuoga mara kwa mara.

b) Kila mwanafunzi anatakiwa kuweka safi mazingira ya darasa, bweni, ukumbi wa chakula kwa

   i) Kushiriki vizuri katika kazi za usafi unapopangiwa

   ii) Kutochafua maeneo hayo kwa njia yoyote ile.

c) Kila mwanafunzi anapaswa kufua nguo na sare zake za shule kila mara.

## I: UKUMBI WA CHAKULA NA JIKO

i) Kila mwanafunzi anapaswa kufika kwenye ukumbi wa chakula kwa wakati uliopangwa na kufuata utaratibu wa kupata chakula

ii) Kila mwanafunzi anatakiwa awe kimya na mtulivu anapopata huduma katika ukumbi wa chakula au jikoni.

iii) Kila mwanafunzi avae kwa unadhifu wakati wa kwenda katika ukumbi wa chakula na jikoni. Nguo za kulalia, viatu vya wazi, ndala havitakiwi kabilsa katika ukumbi wa jikoni.

iv) Ni marufuku kutumia vyombo vya plastic kwa kulia chakula.

v) Lazima kila mwanafunzi afike katika ukumbi wa chakula kwa wakati na kuhudumiwa ndani ya muda uliopangwa. Iwapo utakuja nje ya muda huo hautokuwa na haki ya kudai chakula.

vi) Ni marufuku kwa mwanafunzi kunawa maji na kupiga mswaki karibu na ukumbi wa chakula au jiko.

vii) Ni marufukukubishana na kugombana jikoni au katika ukumbi wa chakula.

## J: MABWENI

i) Kila mwanafunzi anapaswa kushiriki shughuliza usafi wa mabweni naa kuhakikisha umekaguliwa.

ii) Kila mwanafunzi anatakiwa aweke malazi yake katika hali nadhifu kwa kutandika na kupanga vifaa vyake vyote.

iii) Kila mwanafunzi anatakiwa atunze vifaa vyote vya usafi vya bweni husika.

iv) Kila bweni linatakiwa kushiriki katika mashindano ya usafi.

v) Kila mwanafunzi asafishe chumba chake anacholala kila siku.

vi) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki silaha na vifaa hatarishi bwenini kama nondo, nyundo,mkuki,upinde,visu,rungu, bunduki n.k.

vii) Ni marafuku kutunza vifaa vyote vya plastiki bwenini isipokuwa ndoo tu.

viii) Ni marufuku mwanafunzi kujihamisha bweni alilopangiwa na kwenda bweni jingine bila kibali maalum.

ix) Ni marufuku mwanafunzi kumuhifadhi mwanafunzi wa bweni jingine au shule nyingine bila kibali cha Mwalimu wa malezi/mkuu wa shule.

x) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea bweni jingine au kukaa nje ya bweni jingine bila kibali maalumu/utaratibu maalum.

xi) Ni marufuku kumuhifadhi mgeni yeyote bwenini au kufika katika eneo la bweni bila kibali maalumu.

xii) Ni lazima kwa kila mwanafunzi kushiriki usafi wa bweni lake, ndani na nje.

## K: MASIJALA NA UHIFADHI WA KUMBUKUMBU ZA WANAFUNZI

i) Ni lazima mwanafunzi anapofika shuleni kwa mara ya kwanza kuhakikisha anawekwa kwenye kumbukumbu muhimu kwa kuandikishwa katika madaftari ya usajiri, mabweni, madarasa n.k.

ii) Nilazima mwanafunzi ataje na kuandika jina lake sahihi lililo katika kumbukumbu za vyeti vyake vya shule za awali

iii) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuandika jina analolifurahia au la utani au kufanya mabadiliko ya herufi katika jina lake halali.

iv) Ni lazima mwanafunzi ajiorodheshe katika ofisi ya malezi au kamati maalumu ya mapokezi pindi afikapo shule kwa mara yakwanza au arudipo kutoka likizo.

v) Ni lazima mwanafunzi kuthibitisha uwepo wake shuleni kwa kujiorodhesha awapo mstarini,darasani katka kila kipindi, maandalio ya jioni na wakati wowote inapobidi kufanya hivyo.

vi) Ikiwa mwanafunzi hatoweza kujiorodhesha katika maeneo yote tajwa hapo juu kutokana na ugonjwa n.k, atoe taarifa lasimi yenye vithibitisho kwa mkuu wa shule.

vii) Ni lazima mwanafunzi aitwe jina kabla na baada ya kipindi cha Mwalimu kuisha.

## L: MAWASILIANO

Mawasiliano ni jambo muhimu sana kwa binadamu yeyote. Mawasiliano holela hayaleti ustawi wa kimaendeleo badala yake hubomoa.

Shule ina mpangilio na utaratibu wa mwanafunzi kuwasiliana na mzazi au mlezi au yeyote nje ya shule

Utaratibu huu hutolewa na kuelezwa kwa mwanafunzi mara anapo ripoti shuleni ili ufuatwe.

Kwa mantiki hiyo, ***Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu ya mkononi shuleni. Mwanafunzi atakae kamatwa na simu atanyang'anywa na haitarudishwa au Itaharibiwa hapohapo, pia atapewa adhabu nyingine, ikiwemo kufukuzwa shule.***

## M: WAGENI

a) Mgeni yeyote wa mwanafunzi ni lazima kuripoti kwa mwalimuwa zamu au ofisi za utawala wa shule kabla ya kukutana na mwanafunzi alitembelewa.
b) Mwanafunzi haruhusiwi kumpokea mgeni yeyote katika mazingira ya shule bila waalimu kuwa na taarifa.
c) Mwanafunzi haruhusiwi kumpeleka mgeni yeyote ofisini, darasani au bwenini.
d) Mwanafunzi hatoweza kuonana na mgeni aliemtembelea kama mgeni huyo atafika shuleni zaidi ya saa 12:00 jioni.
e) Ni marufuku kwa mwanafunzi wa shule nyingine kutembelea shuleni zaidi ya saa 12:00 jioni kwa kisingizio chochote kile.
f) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukaa na kudhurula ndani ya eneo la shule bila kibali cha utawala wa shule.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Kuunganisha umeme isivyo halali katika majengo ya shule.
4. Matumizi ya madawa ya kulevya na ulevi
5. Uvutaji bangi
6. Makosa ya jinai
7. Kupigana na kupiga
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya mwanafunzi mwenzie,mfanyakazi au mali ya umma.
9. Kudharau bendera ya taifa au wimbo wa taifa.
10. Kuoa/kuolewa
11. Kusababisha mimba ndani ya jamii ya shule au nje ya jamii ya shule.
12. Kutoa mimba
13. Kumdharau kiongozi au kumpiga.
14. Kumdharau Mwalimu au mtumishi asie Mwalimu,kumdhalilisha, kumtishia au kumpiga.
15. Kugoma, kuchochea migomo,kuongoza migomo,kuvuruga amani,usalama na utulivu wa shule na jumuiya zilizopo shuleni.
16. Kwenda nje ya shule bila kibali maalumu cha shule.
17. Kukataa adhabu kwa makusudi anayoadhibiwa na Mwalimu.
18. Kupiga makelele usiku ukivuruga wanafunzi wanaojisomea au usingizi wao.

**MKUU WA SHULE**